MUHUTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA UCHUMI

YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika,

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uzima na afya njema na kuweza kufika hapa leo hii kwa ajili ya shughuli zetu za ujenzi wa Taifa letu. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye niweze kuusoma muhutasari huu wa Ripoti ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022 kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa dhati kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe muhutasari huu wa Ripoti ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika,

Tunatoa pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavoiongoza nchi yetu kwa busara na kuendelea na juhudi za kuweka misingi ya uchumi kupitia sekta ya Uwekezaji na kuitumia vyema rasilimali bahari kupitia sera ya Uchumi wa Buluu ambayo imejipatia umaarufu mkubwa. Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi inaunga mkono juhudi hizo na tunamuomba Mola mtukufu atujaaliye mafanikio katika utekelezaji wake ili kuinua hali za wananchi kiuchumi.

Aidha, tunampongeza sana Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa msaada mkubwa anaompatia Mheshimiwa Rais katika uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika,

Kamati ya Uchumi ni miongoni mwa Kamati nane za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 107, Jadueli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Kamati hiyo imepangiwa kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na ya Wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambuwa mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambuwa ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Katika utekelezaji wa kazi zake, Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kutatua changamoto hizo.

Kamati ya Uchumi inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara tatu zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Afisi ya Rais, Fedha na Mipango
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,**

Ni ukweli usiopingika kuwa Wizara zote hizi ndio kiini cha uchumi wa nchi yetu. Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi, Makatibu wakuu pamoja na Watendaji wao wote kwa namna wanavyoipatia ushirikiano Kamati kila inapohitajika. Juhudi zao ndizo zilizowapa hamasa Wajumbe ya kuweza kuuliza na kupata uelewa mpana wa masuala mbalimbali ya Uchumi ambayo yatawasaidia katika utungaji wa Sera na Sheria mbali mbali kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mara nyengine tena napenda kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa mashirikiano ya hali ya juu waliyoyaonesha wakati wote wa kazi za Kamati ambayo yamewezesha kufanya shughuli zetu kwa wepesi. Naomba niwaarifu Wajumbe wa Baraza hili majina halisi ya Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Juma Makungu Juma - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe
8. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Naomba pia niwataje Makatibu wa Kamati hii:

1. Ndg. Nouman Thabit Nouman - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

## AFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali haziyumbi ingawa uchumi wa dunia umeathiriwa na janga la UVIKO – 19. Ni jambo la kutia moyo kuona mambo yote ya msingi yanaendelea na huku tukitafuta njia mbadala za kuimarisha uchumi wetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021, jumla ya shilingi 440.59 bilioni zilikusanywa kutoka katika vyanzo tofauti vya mapato ikiwemo sekta ya utalii, kodi zinazotokana na biashara, mapato yasiyokua ya kodi na mchango kutoka kwa washirika wa maendeleo, sawa na asilimia 72 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Disemba 2021, Kamati iliarifiwa kuwa matumizi halisi ya Wizara yamefikia jumla ya shilingi 116.13 bilioni sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Matumizi hayo yanajumuisha shilingi 22.58 bilioni ambayo ni matumizi ya fungu F01 (OR - Fedha na Mipango) ambayo ni sawa na asilimia 35 za makadirio ya shilingi 64.77 bilioni; shilingi 86.73 bilioni kwa ajili ya matumizi ya fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali) ambayo ni sawa na asilimia 89 ya makadirio ya shilingi 97.09 bilioni na shilingi 5.02 bilioni kwa ajili ya matumizi ya (fungu F03) Tume ya Mipango, ambayo ni sawa na asilimia 49 ya makadrio ya shilingi 10.31 bilioni.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilipitisha Mswada Wa Sheria Ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Uanzishwaji wa Ofisi hii ni hatua muhimu katika kusimamia utekelezaji wa Taasisi za uwekezaji za umma na mali za umma. Hatua hii ni muhimu katika kuimarisha utawala bora nchini. Tunaipongeza Serikali kwa hatua hii muhimu tuliyoifikia ambayo inajenga nidhamu ya matumizi ya umma kwa kuweka usimamizi wa moja kwa moja kupitia uanzishwaji wa Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongezi kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa kuanza rasmi matumizi ya mashine za kielektroniki (VFMS Disemba, 2021) na (VFD Januari, 2022). Hatua hiyo ni muhimu katika kuziba mianya ya makusanyo na kuzitumia fedha hizo kwa ajili ya shughli za ujenzi wa Taifa letu. Hata hivyo, Mwamko mdogo wa wananchi juu ya suala zima la kudai risiti kila wanapofanya manunuzi hata baada ya kuanza matumizi ya mfumo wa kielektroniki unarejesha nyuma zoezi zima la matumizi ya mashine hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Bodi ya Mapato Zanzibar kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kudai risiti na namna inavyochangia kwenye maendeleo ya nchi yetu.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ni shughuli muhimu ambayo Serikali yetu imeamua kwa umuhimu wake kuianzishia mamlaka maalum. Hii ni Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar iliyoundwa kwa sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuunda chombo hiki na inashauri changamoto ya usafiri waliyonayo itatuliwe ili kuleta ufanisi

katika kazi. Aidha, maslahi ya watendaji wa taasisi hii yanapaswa kuangaliwa upya ili kuwalinda na vishawishi vinavyoweza kutokea katika shughuli zao za kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Taratibu za uondoshaji wa mali za umma zimeelezwa na sheria ya Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Kamati yangu imesikitishwa sana kuona baadhi ya taasisi za umma zinakiuka sheria hiyo kwa kugeuza sehemu ya taasisi zao kuwa ni mafichio ya vifaa chakavu na hivyo kuchafua mazingira ya ofisi hizo. Kwa mnasaba huo tunaiomba Serikali isimamiye vyema utekelezaji wa Sheria hii kwa taasisi zote ili tupate tija iliyokusudiwa kwa utungwaji wake.

**TAASISI ZINAZOJITEGEMEA**

Mheshimiwa Spika, Afisi ya Rais Fedha na Mipango inasimamia Taasisi nane (08) zinazojitegemea na Taasisi nne (04) za Muungano zinazofanya kazi hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Benki ya watu wa Zanzibar ni benki inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ilianzishwa mwaka 1966 kwa ajili ya kuhudumia Serikali na wananchi wake. Hadi sasa, benki ina jumla ya matawi 16, Vituo 6 vya kutolea huduma, mashine 35 za kutolea fedha (ATM), maduka 6 ya kubadilishia fedha na mawakala 266 katika mikoa mbalimbali ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**

Ingawa PBZ imeingia kwenye ushindani na benki nyengine za biashara nchini, benki hiyo inashindwa kwenda sambamba na wakati kutokana taratibu za manunuzi na kuendeshwa kwa mfumo wa Idara kama Idara nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, jambo ambalo hupelekea kushindwa kufanya maamuzi ya haraka yatakayoipatia benki faida kubwa. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuiandalia mazingira mazuri benki hii ya kufanya maamuzi ya

kibiashara kwa haraka. Aidha, watendaji wa juu wa benki hii wanapaswa kuitumia fursa hiyo kwa uadilifu kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili kuzitumia vyema fursa za kibiashara, Serikali haina budi kuiwezesha benki ya watu wa Zanzibar kwa kuitengenezea mifumo itakayofanikisha majukumu yote makuu ya Kitaifa kama bank Insurance na mfumo wa kuweza kuzihudumia fedha za ahueni ya UVIKO - 19. Jambo hili litaipa heshima kubwa PBZ na kutengeneza faida nzuri.

**Mheshimiwa Spika,**

Sekta ya fedha nchini ndio chachu ya maendeleo ya kiuchumi. Kwa mnasaba huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeunda Benki Kuu ya Tanzania (BOT) chini ya sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Namba 4 ya mwaka 2006 kwa ajili ya usimamizi wa sekta hiyo. Kamati yangu inaiomba Serikali kuu kuingilia kati kadhia ya kufungwa kwa benki ya FBME na kutafuta namna bora ya kuwapatia haki zao wananchi wenye akiba kwenye benki hiyo. Jambo hilo litarejesha imani ya wananchi kwa Benki Kuu na Serikali yao.

Kamati pia inaiomba Serikali kupitia BOT kuwaelewesha wananchi juu ya fursa za uwekezaji katika masoko ya fedha kwani imebainika kuwa Wananchi walio wengi hawana uelewa huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeundwa kwa sheria namba 11 ya mwaka 1995 na imeanza kazi rasmi mwezi wa Julai mwaka 1996 ikiwa na jukumu kuu la kusimamia ukusanyaji wa kodi na ada mbalimbali zinazotozwa na Serikali Kuu. Kwa upande wa Zanzibar, ofisi ya TRA inaongozwa na Naibu Kamishna na ina jumla ya Watendaji 167, kati yao wanawake 47 na 120 ni Wanaume.

Kamati yangu ilitembelea Mamlaka hiyo na kubaini changamoto kadhaa zinazokwaza utendaji wake kama ifuatavyo:

1. Uchelewaji wa utatuzi wa migogoro ya kodi katika ngazi ya mahakama za kodi katika kesi zinazotokea baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipa kodi mbali mbali.
2. Watumishi wapya wa Mamlaka ya Mapato Tanzania hawana ujuzi wa kutosha katika fani za utozaji wa kodi kwa kampuni zinazofanya kazi kati ya Zanzibar na nchi za nje (international taxation). Kasi ya kustaafu wataalamu wabobezi haiendani na kasi ya uajiri. Hivyo TRA inakabiliwa na uhaba wa watendaji wenye ujuzi.
3. Ufinyu wa nafasi katika bandari ya Zanzibar unapelekea msongamano wa meli za mizigo zikitokea katika bandari ya Mombasa Kenya na Bandari ya Dar-es-salaam na kupelekea kupungua kwa kasi ya uteremshaji wa makontena na hivyo kuathiri mzunguko wa biashara na malipo ya kodi.
4. Mwamko mdogo wa ulipaji wa kodi kwa hiari baina ya wananchi

Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuzitatua changamoto hizo kwa maendeleo ya Mamlaka yenyewe na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii Zanzibar (ZSSF) na kupatiwa taarifa juu ya ulipaji wa mafao mbali mbali pamoja na shughuli za uwekezaji zinazoendeshwa. Jumla ya shilingi 617,682,716,263.83 bilioni zimewekezwa na mfuko kwenye maeneo mbali mbali ya kiuchumi ili kutengeneza faida na kuweza kumudu gharama za uendeshaji.

Kutokana na janga la mripuko wa UVIKO-19, baadhi ya waajiri wamepunguza wafanyakazi wao raia wa kigeni. Mfuko ulitarajia kulipa marejesho kwa wanachama 187 lakini waliolipwa ni wanachama 121 sawa na 64%, jumla ya shilingi 1,497,722,905 bilioni zilitarajiwa kutumika kama marejesho lakini zilitumika shilingi 1,668,378,160 bilioni ambazo sawa na 111% .

Uwekezaji wa mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwenye baadhi ya miradi haujenda vizuri kutokana na sababu mbali mbali. Hivyo, Kamati inashauri Mfuko kutafuta maeneo ya kimkakati kwa ajili ya kuwekeza ambayo yatakuwa na uhakika wa kupata marejesho kwa muda mfupi na kuendeleza ustawi wa mfuko na wanachama wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Tukijikita katika suala zima la usimamizi wa huduma za bima nchini, Serikali imeunda Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa ajili hiyo. Kamati yangu iliitembelea Mamlaka hiyo na kuelezwa namna inavyoendesha shughuli zake. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Mamlaka inaendelea kutekeleza Mkakati wa miaka mitano wa Uendelezaji soko la Bima (TIRA –Corporate Strategic Plan 2020 – 2025). Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, Mamlaka imeandaa mkakati wa upelekaji wa elimu kwa umma wa miaka minne (National Insurance Education Srtategy – 2021- 2025) ambao utapelekea asilimia 78 ya wananchi kupata uelewa wa masuala ya bima. Hadi kufikia 2029/30, watumiaji wa huduma za bima nchini wataongezeka kutoka asilimia 15 ya sasa hadi kufikia asilimia 50. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa hatua zinazochukuliwa na Mamlaka hii na inatoa wito kwa Mamlaka nyengine kufanya juhudi na maarifa ili kuhakikisha malengo ya kuasisiwa kwake yanatimia.

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto kuu zinazoikabili Mamlaka ni Kutokuwa na kampuni ya bima inayotoa huduma ya bima ya Kimataifa ambapo baadhi ya wateja waliopo nchini wanahitaji huduma hiyo, Kutokuwa na sera ya Bima ya Taifa pamoja na kutokuwa na Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ambayo ndio chombo kikuu cha maamuzi ya taasisi ambacho kimekosekana tangu mwaka 2019 hadi pale wakati Kamati ilipoitembelea taasisi hiyo. Kamati inaiomba Serikali kuzitafutia suluhu changamoto hizo ili kuendelea na utendaji bora wa taasisi hii.

Aidha, Kamati inaiomba Serikali kupitia (TIRA) kuipitia upya Investment ratio ya mashirika ya Bima nchini na kupunguza kiwango hicho ili kuyapa nafuu mashirika hayo na kuyafanya yapate maendeleo ya haraka.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa hapa Zanzibar, huduma za bima zilianza kutolewa tangu mwaka 1969 mara baada ya kuanzishwa Shirika la Bima la Zanzibar. Shirika hilo ni shirika la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lililoanzishwa mwaka 1969 na linaendeshwa kwa mujibuwa sheria ya Mitaji ya Umma Namba 4 ya mwaka 2002. Kamati ya Uchumi imeridhishwa na utendaji wa Shirika hili mara baada ya kulikagua makao makuu na kwenye matawi yake mbali mbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili Shirika litengeneze faida kutokana na biashara ya bima, Kamati inazitaka taasisi za umma na za binafsi kulipa madeni yake yote. Katika kufanikisha azma hii, Shirika liziandikie barua za ukumbusho taasisi zenye madeni makubwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuifanyia marekebisho sheria ya "Motor Vehicle Third Party Risk Decree Cap 136" ambayo ilitungwa mwaka 1953 na kubainika kuwa viwango vya adhabu zake vimepitwa na wakati na vinalikosesha Shirika Mapato.

## AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya Idara 8, Ofisi Kuu Pemba na taasisi 2 zinazojitegemea. Kamati yangu haitosita kuipongeza Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mashirikiano wanayoipatia wakati wote wa shughuli za Kamati.

Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2021 Wizara ilitarajiwa kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi 1,463,126,000 bilioni lakini imefanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 654,982,926 milioni sawa na asilimia 45 ya lengo kutokana na Ada za

Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi na Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi. Kamati inaagiza Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhakikisha inakusanya zaidi ili kuchangia kwenye pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Matumizi ya Afisi hii yamegawika katika mafungu mawili ya kibajeti na yanasimamiwa na Makatibu wakuu wawili.

Kwa Kipindi cha Julai – Disemba 2021 Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 3,844,937,795 bilioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 877,236,820 milioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote, shilingi 845,650,477 milioni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Shilingi 2,122,050,498 bilioni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Kiuhalisia, jumla ya shilingi 2,294,605,336 bilioni ziliiingizwa na kutumika sawa na asilimia 60 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwezeshaji) Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,427,912,000 bilioni kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,261,447,000 bilioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na shilingi 166,465,000 milioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Kiuhalisia jumla ya shilingi 707,636,115 milioni sawa na asilimia 50 ya makadirio.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo zimeundwa kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa ajira za staha pamoja na kuhakikisha viwango vya kazi ili kuimarisha usalama na afya kazini. Kamati imesikitishwa na uhaba wa vyombo vya usafiri unaopelekea kazi ya kufanya ukaguzi kufanyika kwa kusuasua. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala zima la vyombo vya usafiri kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo ya kazi ili kurahisisha shughuli za Kamisheni ya Kazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Suala la kutokua na utaratibu mzuri wa uwekaji wa taarifa *(Database System)* kwa Kamisheni ya Kazi ambayo ndio chombo cha kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi katika sekta binafsi kwa hapa Zanzibar limeitia wasiwasi Kamati. Hali hii itawasababishia vijana wetu wanaofanya ajira za muda kuendelea kupata misukosuko ya kuondolewa kazini mara kwa mara.

Ni jambo la busara Kamisheni ya Kazi ikaandaa mwongozo wa ajira za muda mfupi ambao utafuatwa na taasisi zote nchini. Kitendo hichi kitawafanya vijana wetu kuwa na uhakika wa ajira kwa muda wa mkataba husika. Aidha, Kamisheni ipewe mamlaka ya kufuatilia ajira za taasisi binafsi ili kuhakikisha miongozo ya Serikali inafuatwa katika suala la uajiri.

## PROGRAMU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalenga kuwaondolea wananchi hali ngumu ya kimaisha kwa kuwafanyia program mbalimbali za uwezeshaji.

Programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inahusika na Utoaji wa Huduma za Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo ili waanzishe na kuendeleza Miradi yao ya Kiuchumi itayowapatia kipato cha kujikimu kwa maisha yao ya kila siku na ya familia zao. Kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2021 Mfuko umetoa mikopo 248 (Unguja 136 na Pemba 112) yenye jumla ya Shilingi 210,050,000 milioni.

Kamati iliarifiwa kuwa mfuko ulishiriki kikamilifu katika kufanikisha maonesho ya wajasiriamali wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliyofanyika Mwanza Tanzania. Jumla ya wajasiriamali 18 kati ya 46 wa Zanzibar walioshiriki maonesho hayo ni wateja wa Mfuko. Kupitia maonesho hayo wajasiriamali wetu wamepata uzoefu na wamejifunza kutoka miongoni mwao. Pia, wamepata fursa ya kubadilishana bidhaa katika nchi tofauti zilizoshiriki, jambo ambalo limepelekea kuzitangaza bidhaa zao na kujenga ukaribu baina ya wajasiriamali wa ndani na nje ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na jitihada za mfuko huu, wajasiriamali walio wengi hawana muono wa mbali jambo ambalo hupelekea kutotumia kikamilifu fursa za kukua kibiashara zinazotokea kwa upande wao na kuendelea kuwa duni kimaisha wao na familia zao. Pia, Kamati imebaini kuwa wajasiriamali wengi hawana taarifa sahihi juu ya fursa za mikopo na hivyo wanashindwa kuzitumia kwa maendeleo ya shughuli zao. Hivyo, Kamati inaishauri Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kulifanya suala la elimu kwa jamii kuwa ni ajenda maalum ili kuongeza uelewa wa wananchi hao katika mambo haya.

**Mheshimiwa Spika,**

Nchi yetu inatunga sheria na sera mbalimbali ili kuwanufaisha wananchi wake. Kamati yangu imebaini mapungufu kwenye usimamizi wa Sera ya biashara huria ambayo inawaumiza wazalishaji wadogo wadogo kwani baadhi yao huzalisha na kuuza kwa bei ya chini ilhali bidhaa ileile inauzwa kwa bei ya juu na mtu wa kati sokoni. Matokeo yake ni kupata maendeleo makubwa mtu wa kati bila ya gharama yoyote na kumuacha mzalishaji akiwa na hali duni ingawa yeye ndiye aliyeumiza kichwa kubuni biashara yake,

kuitengeneza na kuiingiza sokoni. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara inayoshughulikia mambo ya biashara kulisimamia hili kwa maslahi ya wajasiriamali wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imeridhishwa na harakati za kuikomboa jamii kupitia akinamama wanyonge zaidi wa vijiji vya Unguja na Pemba kupitia mradi wa Barefoot.

Barefoot ni mradi wa nishati mbadala ya umeme wa jua ambao umeanzishwa nchini mwaka 2015 kwa ajili ya kuwapatia umeme wananchi masikini ambao hawana uwezo wa kugharamia huduma ya umeme wa kawaida. Mradi umeanzisha kituo maalumu cha mafunzo (barefoot college) kilichopo Kinyasini Unguja ambacho kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa ni kati ya vituo 20 bora vya aina hiyo duniani. Mradi unatekelezwa pia kwa upande wa Pemba ambapo umeanza rasmi mwaka 2017 katika kijiji cha Makoongwe. Mbali na huduma hiyo ya umeme wa jua, kituo pia kinawapatia akinamama ujuzi wa shughuli mbali mbali za biashara ikiwemo mafunzo ya ufugaji wa nyuki na ushoni.

**Mheshimiwa Spika,**

Changamoto kuu za mradi huo ni upungufu kwa kipato cha Mradi kila Mwaka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupatikana kwa huduma ya umeme wa kawaida kwenye vijiji mbalimbali nchini hadi kufikia hatua ya kukosekana kabisa fedha za kuwalipa solar mamas kwa ajili ya kazi zao. Kwa mfano katika kijiji cha Makoongwe, hadi kufikia mwezi Agosti 2021, mradi ulifanikiwa kupachika Solar 50 tu na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 36,000 tu kati ya shilingi 2,400,000 zilizokadiriwa. Kadhalika, Ufinyu wa bajeti unapelekea akinamama wanaomaliza mafunzo kubaki bila ya kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi kwa muda mrefu. Pia, uelewa mdogo wa wanajamii juu ya umuhimu wa mradi ni suala la kutiliwa maanani sana na kuwapatia uelewa huo wananchi kwa maslahi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili kuendeleza mradi huu kwa ufanisi, Kamati yangu inaishauri Wizara kujikita katika kutoa elimu kwa wananchi ili kujua faida mbali mbali zinazotokana na Mradi huu na kusaidia kuulinda na kuuimarisha mradi huo. Aidha, tunaiomba Serikali kukitunza na kukiendeleza kituo hiki cha mafunzo ili kiwe chachu ya mafanikio kwa akinamama ambao ndio tegemeo kwa familia zao.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inalenga kuimarisha uchumi kupitia mashirikiano baina ya sekta za umma na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo. Uwekezaji ni njia mojawapo inayotumiwa katika kufanikisha malengo hayo. Jukumu hili linatekelezwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) ambayo ni Taasisi ya Serikali inayofanyakazi chini ya Sheria ya Mamlaka ya kukuza na kulinda Uwekezaji Zanzibar Na. 14, 2018.

Serikali, kupitia Mamlaka hii imeelekeza nguvu zake katika kutangaza na kusimamia Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2008 katika sekta zote zinazohusika. Aidha, mkazo maalum umewekwa kwenye uimarishaji wa uchumi wa buluu ikizingatiwa kuwa jiografia ya Zanzibar ni visiwa na ina uwanja mpana wa kuimarisha sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwa safari yetu ya kukuza uwekezaji inakabiliwa na changamoto za kisera na za kibiashara hususan kwenye miradi inayohusu uzalishaji wa bidhaa. Wawekezaji hukumbana na kodi mbali mbali zinazowafanya kushindwa kuingiza bidhaa zao kwenye soko la Tanzania Bara jambo ambalo linawanyima fursa ya kukuza miradi yao. Kutokana na hayo, Kamati inaiomba Serikali yetu sikivu kufanya mazungumzo na

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwaruhusu wawekezaji wa Zanzibar kuingiza bidhaa kwenye soko la Tanzania Bara kama ambavyo wawekezaji wa Tanzania bara wanavyoingiza bidhaa zao Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza Wizara kupitia ZIPA kwa kutekeleza kwa vitendo dhana ya "one stop centre" kwa asilimia kubwa ndani ya ofisi za ZIPA, na inaishauri Serikali kupitia Wizara husika kuwapa uwezo maafisa wake wa kufanya maamuzi yote yanayohusiana na shughuli za taasisi zao hapo hapo ili kuepusha maombi ya wawekezaji kuchukua muda mrefu kusubiri maamuzi.
Aidha, Kamati inaipongeza PBZ kwa kuanza kuudumia kituo hichi cha "one stop centre" ili kurahisisha masuala yote ya malipo na kukamilisha dhana nzima ya uanzishwaji wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali yetu imejikita kwenye sekta ya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali kwa nia ya kuongeza ajira kwa vijana na kuifungua nchi yetu kiuchumi. Tunaipongeza Serikali kwa azma yake hiyo njema na Tunaomba viongozi waliopewa dhamana ya kulisimami suala hili walisimamie kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati yangu imesikitishwa na baadhi ya wawekezaji hao kuitumia vibaya fursa waliyopewa na kwenda kinyume na nia njema ya Serikali kwa kuwasilisha miradi inayokubalika mbele ya ZIPA na kupatiwa ruhusa lakini hatimaye hushindwa kuendelea na miradi hiyo kwa sababu mbalimbali.

Kamati yangu imeshuhudia baadhi ya wawekezaji hao wakiwa na maeneo makubwa ya ardhi ambayo wameyahodhi kwa muda mrefu bila ya kuyafanyia uwekezaji waliokubaliana na Serikali na hivyo kuwakosesha wawekezaji waliokuwa tayari maeneo yakutosha ya kuwekeza (land bank). Wawekezaji hao hufanya taratibu za kupata nyongeza ya ardhi kinyume na taratibu na bila ya kupitia kwenye Mamlaka husika ya Uwekezaji (ZIPA) na kuwa na khulka ya kubadilisha dhana ya mradi mara kwa mara jambo ambalo linapelekea upotevu wa kodi za Serikali kwani mabadiliko hayo hufanywa kila ikikaribia mwisho wa muda wa msamaha wa kodi (*tax holiday).*

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kufanya mapitio ya sheria zake na iwapo kuna sheria inayotoa mwanya kwa wawekezaji hawa na kuwalinda iletwe mbele ya baraza hili kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ili hatua za kuwanyang'anya ardhi ziendelee na kukabidhiwa kwa wawekezaji wenye nia ya dhati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na malalamiko ya Wawekezaji wa sekta ya ujenzi nchini kuwa miradi yao haiwezi kuwaletea tija kwa kutozingatiwa maslahi ya mnunuzi wa nyumba hizo (*buyer's benefits*), Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwapa kazi maalum wataalamu wa ZIPA kufanya uchambuzi wa kitaalamu (*due diligence*) ili kujiridhisha ni faida gani itakayopatikana kwa nchi yetu iwapo tutaondoa kodi zote zinazotokana na mauzo ya nyumba hizo kwa mujibu wa matakwa ya wawekezaji.

## WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021,Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,418,118,000 bilioni ambapo ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 623,389,989 milioni sawa na asilimia 43.9 ya makadirio.

Aidha, Kwa kipindi chaJulai hadi Disemba 2021, Wizara pamoja na taasisi zake zote iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 3,246,091,429 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuipatia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi jumla ya shilingi 36.5 bilioni kutokana na

fedha za ahueni ya UVIKO - 19, kwa ajili ya kuwawezesha wadau wa sekta ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya Baharini.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2021, Kamati imearifiwa kuwa, Wizara imesaini jumla ya mikataba kumi na mbili (12) kupitia Kampuni saba (7) katika mchakato wa kufanya matumizi sahihi ya fedha hizo kama ifuatavyo:

a) Mikataba ya kampuni tano (5) za kutengeneza boti 300 za Uvuvi zenye urefu wa mita saba (7) ambapo kila boti moja itagharimu Dola za Marekani U$D 10,580 sawa na shilingi24.3Milioni. Hivyo boti zote 300 kwa ujumla zitagharimu jumla ya shilingi7.3 Bilioni.

b) Mikataba ya kampuni nne (4) za kutengeneza boti 277 za Uvuvi zenye urefu wa mita nane (8) ambapo kila boti moja itagharimu Dola za Marekani U$D 13,800 sawa na shilingi 31,740,000milioni. Hivyo boti 277 kwa ujumla zitagharimu jumla ya shilingi 8.79 bilioni.

c) Kampuni moja imepatiwa mkataba wa kuipatia Wizara vifaa vya wakulima wa mwani vikiwemo tai tai na kamba za aina zote zinazohitajika katika ukulima wa mwani. Aidha, wakulima wa mwani 5000 watapatiwa vifaa hivyo vyenye jumla ya shilingi 1,587,600,000 bilioni.

d) Kampuni moja imepatiwa mikataba miwili inayohusiana na Ujenzi wa Mabwawa 100 ya Ufugaji wa majongoo bahari yenye thamani ya shilingi 465,727,000 milioni na mkataba wa Ujenzi wa Mabwawa 60 ya ufugaji wa kaa kwa Unguja na pemba wenye thamani ya shilingi 264,270,000 milioni.

**Mheshimiwa Spika,**

Sekta ya mafuta na gesi asiia ni mpya hapa Zanzibar na inahitaji kuendelezwa vyema ili iweze kuleta tija kwa nchi yetu. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuanzisha chombo cha udhibiti wa rasilimali hizo ambacho ni Mamlaka Ya Kudhibiti Utafutaji Na Uchimbaji Wa Mafuta (Zanzibar Petroleum (Upstream) Regulatory Authority) (ZPRA)
chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia nambari 6 ya Mwaka 2016. Mamlaka hii imeanza kazi rasmi mwezi Machi 2017 kufuatia kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka. Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, shughuli kuu ya Mamlaka ni kusimamia na kudhibiti shughuli za Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imeshangazwa na kitendo cha kutothibitishwa kwa muundo wa Mamlaka hii na Kamisheni ya Utumishi wa Umma jambo ambalo linaleta ukakasi kwenye utendaji wa shughuli za Mamlaka. Aidha, kutokana na hali hiyo maslahi ya watendaji wa Mamlaka hayaendani na uhalisia wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia duniani.
Kwa mnasaba huo Kamati inaitaka Serikali kuiangalia kwa unyeti wake Mamlaka hii na kuupitisha muundo wake haraka iwezekanavyo ili kuipa fursa nzuri ya kutekeleza majukumu yake ya Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na upya wake, Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa wataalamu wabobezi kwenye fani maalum za Mafuta na Gesi Asilia. Hali hiyo inapelekea tafiti za kitaalamu kutofanyika kwa ufanisi. Kamati inashauri Mamlaka ijikite katika kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kuleta ufanisi zaidi. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kutenga fungu maalumu kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi ambapo asilimia Fulani ya

fedha hizo itumike kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wetu ili waweze kusimamia vyema rasilimali hizo kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Maeneo yaliyoonesha matokeo chanya ya tafiti za awali za mafuta na gesi asilia (Kama na Tundauwa) na kushuhudia jinsi maeneo hayo yalivyoachwa bila ya kudhibitiwa na kuanza kuvamiwa na wananchi kwa ajili ya makaazi jambo ambalo linaweza kuigharimu Serikali wakati wa kuzichimba rasilimali hizo. Aidha, uchakavu wa barabara inayoelekea kwenye kisima cha awali cha Tundauwa ni tatizo kwa muendelezo wa rasilimali hizo. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kutoa elimu kwa wanajamii wa Tundauwa na Kama juu ya taratibu za uchimbaji wa mafuta ili kuwatuliza wanajamii hao kutokana na shauku ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia walionayo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuyalinda maeneo hayo dhidi ya uvamizi wa wananchi kwa ajili ya makaazi jambo ambalo linahatarisha usalama wao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwa hadi sasa wataalamu hawajaweza kugundua wapi hasa yalipo mafuta, bali walichoweza kugundua ni ishara tu za uwepo wa mafuta. Hatua hii ni muhimu kwa ajili ya Utafiti wa mbele zaidi wa 3D ili hatimaye hatua nyengine zifuatiye na kufikia uchimbaji wa kisima cha majaribio ili kujua mustakbal wa nchi yetu kwenye rasilimali hizi muhimu.

Kamati inashauri Serikali kandarasi za uchimbwaji wa mafuta na Gesi kukabidhiwa kampuni zenye uzoefu wa shughuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni jambo la kujivunia kwamba nchi yetu imeunda chombo cha kusimamia biashara ya mafuta na gesi asilia ambayo ni Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria Nambari 6 ya Mwaka 2016

ya Mafuta na Gesi Asillia na kusajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Sheria Nambari 15 ya Mwaka 2013.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilijionea namna watendaji wa Kampuni hiyo wanavyokabiliana na ufinyu wa nafasi ya kufanyia kazi. Pia, uhaba wa wafanyakazi ni suala linaloikwaza kampuni kutokana na ukweli kuwa maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi asilia yanahitaji kampuni ya Serikali iliyo imara kwenye Nyanja zote zikiwemo wataalamu wabobezi, miundombinu ya uhakika na teknolojia ya kisasa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuratibu uajiri wa wafanyakazi wa Kampuni hii ili kuleta ufanisi katika kazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Nchi yetu ina fursa adhimu ya kuendelea kupitia sekta ya uvuvi kama zilivyo nchi nyengine za visiwa duniani. Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO), ikiwa ni katika kutekeleza Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050, MKUZA III na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025. Malengo makuu ya kuanzishwa kwa Kampuni hii ni pamoja na "Uvuvi endelevu wa kibiashara, kuimarisha miundombinu ya Uvuvi, kuanzisha viwanda, kuongeza ajira na pato la Taifa kwa kuzingatia malengo na mikakati ya muda mrefu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini pamoja na kukuza Uchumi wa Buluu.

**Mheshimiwa Spika,**

Ingawa Kampuni hiyo imenunua meli ya Uvuvi (sehewa 02) kutoka nchini Srilanka, gharama za mafuta katika kuendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu ni sawa na asilimia 55 za gharama zote za uvuvi wa bahari kuu. Meli hiyo imekua ikihitaji lita 5,500 kwa safari ya wiki mbili sawa na Tsh. 11,418,000 ambazo ni gharama kubwa kulingana na uvuvi unaofanyika. Ili kuiwezesha Kampuni kupunguza gharama za uvuvi na kuongeza faida, Kamati inaishauri Serikali kuzipunguzia kodi za mafuta Boti za Uvuvi za Kampuni.

**Mheshimiwa Spika,**

Uzoefu mdogo wa uvuvi wa Bahari kuu unaendelea kuwa changamoto kwa wavuvi wetu visiwani. Matatizo kadhaa yanaendelea kujitokeza katika safari za uvuvi ikiwemo kujizonga kwa mitego, kuliwa kwa chambo bila ya Samaki kunasa, kukatwa kwa ndoana na kupotea kwa mitego. Kamati inaishauri Kampuni kutoa mafunzo elekezi ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wake hususani mabaharia ambao wanasafiri kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ili kupata mbinu na maarifa ya ziada katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Upatikanaji wa chambo muafaka ni miongoni mwa changamoto kubwa katika uvuvi huu. Aina mbili za Samaki zilitegemewa kutumika kama chambo ikiwemo vibua na ngisi. Ambao upatikanaji wake katika soko la Zanzibar una changamoto zifuatazo ;-

- Samaki hawa wapo sokoni kwa ajili ya matumizi ya chakula kwa hiyo wanauzwa kwa bei ya juu ukilinganisha na samaki wanaouzwa katika masoko ya kimataifa kama chambo. Kwa mfano, kilo ya Ngisi katika soko la Zanzibar ina bei mara mbili ya wale wanaouzwa kutoka nje kama chambo.
- Samaki hawa wanavuliwa kwa kiwango kidogo kwa siku na hivyo inachukua muda mrefu kuweza kukusanya kiwango cha kutosha kinachotakiwa kwa safari ya uvuvi. Hii inaongeza thamani ya chambo kwasababu kuna haja ya kuwahifadhi katika vifaa vya baridi kwa angalau siku saba.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara kutafuta aina nyengine ya chambo ambacho kitapatikana kwenye mazingira yetu kwa gharama nafuu na kupunguza gharama za uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika shughuli zake za msingi, Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi ilikutana na vikundi tofauti vya wakulima wa mwani kikiwemo kikundi cha wema hauozi kilichopo Makangale ambacho kinajishughlisha na ukulima wa mwani kwenye kina kirefu cha bahari baada ya kupatiwa mafunzo na vifaa na Serikali kupitia taasisi ya utafiti na uvuvi na mazao ya baharini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imegundua kwamba kikundi hicho na jamii iliozunguka eneo hilo hawana kabisa elimu inayohusiana na mikopo wala hawajuwi namna ya kujiunga na mifuko ya hifadhi za jamii hususan ZSSF ili wapate manufaa baadae ingawa wanatamani kufanya hivyo. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na ZSSF kutoa elimu kwa jamii yote, inayohusiana na mikopo pamoja na namna ya kuchangia kwa hiyari kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii (ZSSF).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inazitaka Wizara inayohusika na mambo ya Ardhi na maakazi, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara inayohusika na utalii kwenda kwenye eneo la Makangale ili kutatua mgogoro wa njia baina ya mwekezaji mzalendo wa hoteli ya "Pemba Paradise" na wananchi wa eneo hilo kwani Kamati iliarifiwa juu ya mahusiano yasiyoridhisha baina yao jambo ambalo limesababishwa na mwekezaji huyo kuwazuwia wananchi kutumia njia iliyopita pembezoni mwa hoteli yake na kuwalazimisha kuzunguka kwenye njia isiyopitika na kupelekea wananchi kujihisi wanyonge kwenye eneo lao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu na Jumuiya ya Wazazi naomba kuwasilisha.

…………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar**.